Utatu Mtakatifu

“Kuna Mungu mmoja: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, umoja wa Nafsi tatu za milele. Mungu asiyeweza kufikwa na mauti, mwenye enzi zote, mwenye uwezo wote, mwenye kujua yote, juu ya yote, na aliyepo daima. Hana kikomo na anapita ufahamu wa kibinadamu, walakini akijulikana kupitia ufunuo wake mwenyewe. Yu astahili kuabudiwa, kusujudiwa na kutumikiwa na viumbe vyote milele zote.” (Kumb. 6:4; Mt. 28:19; 2Kor.13:14; Efe. 4:4-6; 1Pet. 1:2; 1Tim. 1:17; Uf. 14:7).

Pale Kalvari, karibu kila mtu alimkataa Yesu. Wachache tu walitambua Yesu alikuwa nani kiuhalisi. Mwizi aliyekuwa anakufa aliyemwita Bwana (Luk. 23:42) na askari wa Kirumi aliyesema hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu (Mk. 15:39). Yohana alipoandika alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea (Yoh.1:11), hakumaanisha ule umati uliokuwa Kalvari au taifa la Israeli peke yake walioshindwa kumtambua Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wao. Hili ni tatizo la wanadamu wote kwa kuwa uelewa wao wa Mungu umepungua sana.

Ufahamu wa Mungu

Nadharia nyingi zajaribu kumwelezea mungu na hoja nyingi zikitetea na kupinga kuwepo kwake huonesha kwamba hekima ya mwanadamu haiwezi kupenya Uungu. Kutegemea hekima ya mwanadamu peke yake kumjifunza Mungu ni kama mtu anayetumia lensi kujifunza anga za juu. Hivyo kwa wengi hekima ya Mungu ni hekima iliyofichwa (1Kor.2:7). Kwao Mungu ni siri. Watawala wa dunia hii hawaijui na kama wangeijua wasingemsulubisha Bwana wa utukufu (1Kor.2:8). Mojawapo ya amri za msingi ni kumpenda Mungu kwa moyo wote, roho yote na akili yote (Mt. 22:37 cf Kumb. 6:5). Hatuwezi kumpenda tusiyejua chochote juu yake wala hatuwezi kutafiti kuujua ukuu wa Mungu (Ay.11:7). Je twawezaje kumjua na kumpenda Mwumbaji?

Mungu aweza kujulikana

Kwa kuelewa upungufu wa kibinadamu, Mungu katika upendo na huruma yake, alitufikia kupitia Biblia. Hudhihirisha kuwa ukristo siyo kumbukumbu ya mwanadamu kumtafuta Mungu bal ni kile Mungu alivyojifunua na makusudi yake kwa mwanadamu. Mwana wa Mungu alikuja ili tumjue aliye kweli (1Yoh. 5:20). Na uzima ndio huu, wakujue Mungu wa pekee na kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. (Yoh. 17:3). Hii ni habari njema. Pamoja na kwamba haiwezekani kumjua Mungu kikamilifu, upo uwezekano wa kumjua na kuingia mahusiano naye yanayotuwezesha kuokolewa.

Kupata ufahamu wa Mungu

Elimu ya Mungu ni tofauti na elimu nyingine. Ni suala la kufungua moyo na utayari wa kufanya mapenzi yake na akili. (Yoh. 7:17 cf. Mt. 11:27). Heri walio na moyo safi kwa kuwa watamwona Mungu (Mt.5:8). Wasioamini hawawezi kumjua Mungu. Yuko wapi mwenye hekima … mleta hoja? Mungu alichagua kuwaokoa wanadamu kwa upuuzi wa neno linalohubiriwa (1Kor.1:20, 21). Waliokataa kujiweka chini ya roho walitafsiri vibaya ujumbe wa Mungu kwa upotevu wao.

Kuwako kwa Mungu

Kuna vyanzo viwili vya ushahidi vya kuwako kwa Mungu. Cha kwanza ni kitabu cha maumbile asili na cha pili Maandiko Matakatifu.

Ushahidi wa Uumbaji

Kila moja aweza kujifunza kupitia maumbile asili na uzoefu wa kibinadamu. “Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu na anga latangaza kazi ya mikono yake (Zab.19:1). Ufunuo wa Mungu kupitia maumbile ya asili hutia nuru kila mtu (Yoh. 1:9). Mambo yasiyoonekana yanaonekana kupitia na kufahamika kwa kazi zake (Rum. 1:20). Tabia ya binadamu pia hutoa ushahidi kuwapo kwa Mungu. Paulo asema alihubiri Wagiriki habari za Mungu ambaye wanamwabudu pasipo kumjua (Mdo. 17:23). Tabia ya mwanadamu pia yaonyesha torati iliyoko ndani ya mioyo yao. (Rum.2:14, 15).

Ushahidi wa Maandiko Matakatifu

Biblia haithibitishi kuwako kwa Mungu. Inachukulia kuwa inajulikana. Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi (Mwa. 1:1). Biblia humweleza Mungu kuwa Muumbaji, Mtunzaji na Mtawala wa uumbaji wote. Ufunuo kutokana na uumbaji ni dhahiri sana kiasi kwamba hakuna sababu yoyote kutetea ukafiri (Zab.14:1, Rum. 1:18-22, 28). Upo ushahidi wa kutosha kumshawishi yeyote kujua ukweli kumhusu Mungu. Hata hivyo, imani ni jambo la msingi katika kumjua Mungu maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza (Ebr. 11:1, 6)

Mungu wa Maandiko Matakatifu

Biblia humfunua sifa muhimu za Mungu kupitia majina yake, matendo yake na tabia zake.

Majina ya Mungu

Wakati Maandiko Matakatifu yanaandikwa, majina yalikuwa muhimu kama yalivyo muhimu hata sasa kwa watu wa Mashariki ya Kati na maeneo yanayozunguka. Huko, jina huhesabika kubeba tabia ya aliyepewa hilo jina na utambulisho wake. Umuhimu wa majina ya Mungu, hufunua asili yake, tabia yake, sifa zake na hudhihirishwa na ile amri isemayo: usilijataje bure jina la Bwana Mungu wako… (Kut. 20:7). Daudi aliimba: Nitaliimbia jina la Bwana aliye juu (Zab. 7:17), Jina lake ni takatifu na la kuogopwa (Zab. 119:9); Na walisifu Jina la Bwana, Maana jina lake peke yake limetukuka (Zab. 148:13). Majina ya Kiebrania El na Elohim (Mungu) hufunua uwezo wa kiuungu. Hutoa picha ya Mungu kuwa mwenye nguvu, mwenye uwezo mkuu, Mungu wa uumbaji (Mwa. 1:1; Kut. 20: 2; Dan. 9:4). Elyon (Aliye juu) hulenga sifa ya kuinuliwa (Mwa. 14: 18-20; Isa. 14:14). Adonai (Bwana) hutoa picha ya Mungu kuwa ni mtawala (Isa. 6:1; Zab. 35: 23). Majina haya hukazia tabia ya Mungu ya utukufu usiolinganishwa.

Majina mengine huonesha uhiari wa Mungu kuingia kwenye mahusiano na watu. Shaddai (Mwenye enzi) na El Shaddai (Mungu Mwenye enzi) huonesha Mungu aliye chanzo cha baraka na faraja (Kut. 6:3; Zab. 91:1). Jina Yahweh lililotafsiriwa Yehova au BWANA, hukazia agano la Mungu la uaminifu na rehema (Kut. 15:2, 3; Hos. 12:5, 6). Katika Kutoka 3:14

Yahweh anajieleza kuwa Niko ambaye Niko au Nitakuwa jinsi nilivyo akimaanisha uhusiano wake usiobadilika kwa watu wake. Mara nyingine Mungu amejifunua kwa karibu sana kama Baba (Kumb. 32:6; Isa. 63:16; Yer. 31:9; Mal.2:10) akimwita Israeli “Mwanangu” na “Mzaliwa wangu wa Kwanza” (Kut. 4:22 cf. Kumb. 32:19).

Isipokuwa kwa *Baba*, majina ya Agano Jipya yana maana ile ile ya Agano la Kale. Katika Agano Jipya, Yesu alitumia *Baba* kutuletea sisi uhusiano wa karibu na Mungu (Mt. 6:9; Mk.6:36; cf. Rum. 8:15; Gal.4:6).

Matendo ya Mungu

Waandishi wa Biblia wanatumia wakati mwingi kuandika matendo ya Mungu kuliko Alivyo. Anatambulishwa kama mwumbaji (Mwa. 1:1; Zab. 24:1, 2), anayeushikilia ulimwengu (Ebr.1:3) na Mkombozi na Mwokozi (Kumb.5:6; 2Kor.5:19), akihimili hatma ya mwanadamu. Mungu huweka mipango (Isa.46:11; hutabiri (Isa.46:10), na huahidi (Kumb. 15:6; 2Pet.3:9). Husamehe dhambi (Kut.34:7) and ndiye anayestahili ibada yetu (Uf.14:6, 7). Katika ujumla wake, Maandiko Matakatifu humdhihirisha Mungu kama mtawala (1Tim. 1:17). Matendo yake yamthibitisha ni Mungu mwenye nafsi.

Tabia ya Mungu

Waandishi wa Biblia hutoa habari za ziada juu ya vile Mungu alivyo kwa kutoa shuhuda za tabia ya kiungu.

Tabia za Mungu ambazo hazihamishiki (zisizowalisishwa), yaani tabia za Uungu ambazo haiwezekani zikapewa viumbe walioumbwa. Mungu yupo pasipo kuumbwa, anao uzima ndani yake (Yoh. 5:26). Yu huru kuradhi chochote kwa mapenzi yake (Efe. 1:5), na katika uwezo (Zab.115:3). Mungu ajua vyote (Ayu.37:16; Zab.139:1-18; 147:5; 1Yoh.3:20) kwa sababu akiwa Alfa na Omega (Uf.1:8) anaujua mwisho tangu mwanzo (Isa.46:9-11).

Mungu hupatikana wakati wote na mahali pote (Zab.139:7-12; Ebr.4:13), akipita anga za juu, wakati huo huo akiwa ndani ya kila kitu kwenye anga. Mungu ni wa milele (Zab.90:2; Uf.1:8), akivuka vikomo vya wakati, na wakati huo huo akiwamo katika kila kipengele cha wakati.

Mungu anao uwezo wote. Yaani, hakuna kinachoshindikana kwake hututhibitishia kuwa chochote anachokikusudia, hukifanya (Dan. 4:17; 25, 35; Mt. 19:26; Uf.19:6). Mungu habadiliki kwa sababu ni mkamilifu (Mal. 3:6; Angalia Zab. 33:11; Yak. 1:17). Kwa kuwa tabia hizi humtambulisha Mungu pekee, huwa inamaanisha hazihamishiki.

Ziko tabia zinazohamishika za Mungu, zenye kumjali kwa upendo mwanadamu. Hujumuisha upendo (Rum. 5:8), neema (Rum. 3:24), rehema (Zab. 145:9), uvumilivu (2:Pet. 3:15), utakatifu (Zab. 99:9), haki (Ezr. 9:15; Yoh. 17:25), hukumu ya haki (Uf.22:12) na kweli (1Yoh. 5:20). Karama hizi hutufikia tu kutoka kwa Mtoaji mwenyewe.

Uenyezi wa Mungu

Maandiko Matakatifu hufundisha kwa uwazi uenyezi wa Mungu. "…naye hufanya kama atakavyo, katika jeshi la mbinguni, na katika hao wanaokaa duniani; wala hapana awezaye kuuzuia mkono wake, wala kumwuliza, Unafanya nini wewe?" (Dan. 4:35). "…kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa." (Ufu. 4:11). "Bwana amefanya kila lililompendeza, katika mbingu na katika nchi." (Zab. 135:6). Hivyo Sulemani husema "Moyo wa mfalme huwa katika mkono wa BWANA; kama mifereji ya maji huugeuza popote apendapo." (Mith. 21:1). Paulo, akiutambua uenyezi wa Mungu aliandika: "Nitarejea tena kwenu, Mungu akinijalia. (Mdo. 18:21; Angalia Rum. 15:32), wakati Yakobo anaonya: "Badala ya kusema Bwana akipenda, tutakuwa hai na kufanya hivi au hivi" (Yak. 4:15).

Uteule wa Asili na Uhuru wa Mwanadamu

Biblia hufunua utawala thabiti wa Mungu kwa ulimwengu. Aliwateua tangu asili wanadamu wafananishwe na mfano wa Mwana wake (Rum. 8:29, 30), tufanywe wanawe na kupata urithi (Efe. 1:4, 5, 11). Je, uenyezi wake unamaanisha nini kwa uhuru wa mwanadamu?

Neno kuteuliwa tangu asili maana yake kuamuliwa tangu awali. Wengine wametafsiri kuwa kuna watu ambao Mungu amechagua waokolewe tangu asili, na wengine wameachwa kupotea tangu asili. Paulo, hafundishi mwanadamu yeyote kuachwa na Mungu. Badala yake Mungu hutaka watu wote waokolewe na kujua kweli (1Tim. 2:4). Hapendi yeyote apotee bali walifikie toba (2Pet. 3:9). Hakuna ushahidi wa Mungu kutaka watu wapotee. Hiyo itakuwa kuikataa Kalvari ambako Yesu alikufa kwa ajili ya kila mtu. Ile kila mtu iliyomo katika fungu la "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele" (Yoh.3:16) ina maana yeyote anaweza kuokolewa. Ule uhuru wa mwanadamu ndicho kinachofanya mtu aokolewe au apotee na hii inasisitizwa kwa matokeo ya kutii au kutotii na humhimiza mwanadamu achague utii na uzima (Kumb.30:19; Josh.24:15; Isa.1:16, 20; Ufu. 22:17) na kwa ukweli kuwa inawezekana kwa muumini aliyepata kupokea neema kuanguka na kupotea (1Kor.9:27, Gal. 5:4; Ebr.6:4-6; 10:29)…

Mungu aweza kuona kabla mtu hajachagua, kile atakachochagua na matokeo yake, lakini kujua kabla, hakufanyi Mungu kuhusika na uchaguzi huo. Uteule wa Mungu ni kule kutimiza makusudi ya Mungu kuwa yeyote atakayechagua kumwamini Kristo ataokolewa (Yoh.1:12; Efe. 1:4-10).

Sasa Maandiko yanamaanisha nini yanaposema Mungu alimpenda Yakobo akamchukia Esau? (Rum.9:13) na aliufanya moyo wa Farao kuwa mgumu?(fungu la 17, 18, cf. 15, 16; Kut.9:16; 4:21). Muktadha wa mafungu hayo huonyesha kuwa anachojadili Paulo ni utume siyo wokovu. Wokovu ulikuwapo kwa Yakobo vile vile kwa Esau, ila Mungu alimchagua Yakobo uwe uzao wa kupeleka habari ya wokovu kwa watu wengine. Mungu hutumia uenyezi katika utume wake. Maandiko yanaposema kuwa aliufanya moyo wa Farao kuwa mgumu inampa Mungu utukufu kwa uhuru alioruhusu wanadamu kuwa nao na siyo kwa sababu aliusimika ugumu katika moyo wa Farao.

Ufahamu wa kabla na Uhuru wa Mwanadamu

Ufahamu wa Mungu wa kile mtu anataka kufanya hakuingilii uchaguzi wa wanadamu wa kile wafanyacho, kama vile wanahistoria wanavyojua kilichotokea wakati uliopita hakuingilii kile walichofanya. Kama kamera inavyochukua picha ya tukio pasipo kuingilia kulibadili tukio, ufahamu wa kabla utaliona tukio husika pasipo kulibadili. Ufahamu wa kabla wa Mungu hakuingilii uhuru wa mwanadamu.

Utendaji katika Utatu Mtakatifu

Je, kuna Mungu moja? Vipi kuhusu Kristo na Roho Mtakatifu?

Kuwa Mungu ni moja tu

Kutofautiana na mataifa na mataifa yaliyowazunguka, Israeli waliamini yuko Mungu moja tu

(Kumb.4:35; 6:4; Isa.45:5; Zek. 14:9). Agano Jipya linakazia kuwa Mungu ni moja tu. (Mk. 12:29:32; Yoh. 17:3; 1Kor.8:4-6; Efe. 4:4-6; 1Tim. 2:5). Kuwako Mungu moja tu, hakupingi Utatu Mtakatifu wa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu badala yake kunaondoa wazo tete la kuwako miungu watatu.

Wingi katika Utatu Mtakatifu

Ingawa Agano la Kale halifundishi Utatu Mtakatifu, linaweka uwingi katika Uungu. “Na tufanye mtu kwa mfano wetu” (Mwa.1:26). “Huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu” (Mwa. 3:22). “Haya na tushuke huko, tukawachafulie usemi” (Mwa.11:7). Wakati mwingine Malaika wa Bwana anajitambulisha kama Mungu. Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo” (Kut. 3:2, 6). Rejea mbalimbali humtofautisha Roho wa Mungu na Mungu. Katika kisa cha uumbaji, Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji (Mwa.1:2). Mafungu mengine hutambulisha nafsi tatu katika kazi ya ukombozi. “Bwana Mungu amenituma na roho yake” (Isa.48:16). “Tazama mtumishi wangu, nimetegemezaye; mteule wangu…nimetia roho yangu juu yake…”(Isa.42:1).

Mahusiano katika Utatu Mtakatifu

Kuja kwa Yesu mara ya kwanza inatupatia mwanga kuhusu Utatu Mtakatifu. Injili ya Yohana inatuambia kuwa Utatu Mtakatifu unaye Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wenye mahusiano ya kipekee na usiri.

1. Mahusiano ya Upendano

Yesu alipolia Mungu wangu Mungu wangu mbona umeniacha? (Mk. 15:34), alikuwa akisononekea kutengwa na Baba yake kulikotokana na dhambi. Dhambi ilivunja uhusiano uliokuwapo baina ya Mungu na mwanadamu (Mwa. 3:6-10; Isa.59:2). Katika saa zake za mwisho Yesu asiyejua dhambi alifanyika dhambi kwa ajili yetu, akaonja kutengwa na Baba yake ambalo lilikuwa fungu letu na akafa ikiwa ni matokeo ya kutengwa huko.

Wenye dhambi hawatakaa watambue kifo cha Yesu kilimaanisha nini katika Utatu Mtakatifu. Tangu milele, Yesu alikuwa pamoja na Baba pamoja na Roho Mtakatifu. Waliishi pamoja katika umilele, wakijitolea. Mungu ni pendo (1Yoh. 4:8), inamaanisha kila moja aliishi kwa ajili ya mwenzake na hilo liliwajaza kuridhika na furaha.

Upendo umetafsiriwa katika 1Wakorintho 13. Wengine watashangaa kwa nini uvumilivu na subira vitajwe katika Utatu Mtakatifu. Subira ilihitajika wakati wa kushughulika na malaika walioasi na baadaye wanadamu waliotanga mbali. Hakuna umbali kwa washirika wa Utatu Mtakatifu. Wote ni Mungu, na wanashirikiana mamlaka na sifa. Kwa wanadamu, mamlaka kuu hushikwa na Mwenyekiti au Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni (President), lakini katika Utatu, mamlaka ya mwisho iko kwa washirika wote wa Utatu.

Wakati Mungu siyo nafsi moja, Mungu ni moja katika makusudi, akili na tabia. Umoja hauharibu nafsi nafsi tofauti wala kutofautiana kwa nafsi hakuharibu ukweli kwamba Mungu ni mmoja, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

2. Mahusiano ya kutenda kazi

Katika utatu, utaratibu wa kufanya kazi kwa mgawanyo upo. Mungu halazimiki kufanya kazi mara mbilimbili. Utaratibu ni kanuni inayotawala mbinguni na Mungu hutenda kazi kwa utaratibu. Kuwepo utaratibu kunadumisha umoja katika Utatu Mtakatifu. Baba aonekana kama chanzo, Mwana kama mpatanishi, na Roho kama mwezeshaji au mwenye kufanya kitumike. Yesu kufanyika mwili ni kielelezo bora kuelezea utendaji wa Mungu. Baba alimtoa mwanawe, Yesu akajitoa mwenyewe na Roho akafanya Yesu azaliwe (Yoh.3:16; Mt. 1:18, 20). Ushuhuda wa malaika kwa Mariamu huonyesha matendo ya Utatu: “Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, nguvu zake Aliye juu zitakufunika… hicho kitakachozaliwa kitaitwa Kitakatifu (Luk. 1:35).

Kila mshirika kwenye Utatu Mtakatifu alikuwako wakati wa ubatizo wa Kristo. Baba akitia moyo (Mt. 3:17), Yesu akijitoa mwenyewe kubatizwa ili kuwa kielelezo (Mt. 3:13-15) na Roho akijitoa kumwezesha Yesu (Luk. 3:21, 22).

Karibu na mwisho wa maisha yake duniani, Yesu aliahidi kumtuma Roho Mtakatifu kuwa msaidizi na mshauri (Yoh. 14:16). Saa chache baadaye alilia Mungu wangu Mungu wangu, mbona umeniacha? (Mt. 27:46). Katika saa hizo za historia ya wokovu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu walihusika.

Sasa hivi Baba na Mwana wanatufikia kupitia Roho Mtakatifu (Yoh. 15:26). Mzigo mkubwa wa Utatu ni kumtuma Roho amfunue Baba kwa kila mtu (Yoh.17:3), na kumfanya Yesu awepo kwa uhalisi (Mt. 28:20 cf. Ebr.13:5). Waumini wanateuliwa kwa wokovu kwa ufahamu wa asili wa Baba, wanatakaswa na Roho na kunyunyizwa damu ya Yesu (1Pet.1:2).

Baraka ya Mitume inajumuisha Nafsi zote tatu: “Neema ya Bwana Yesu Kristo, na Pendo la Mungu na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote” (2Kor.13:14). Kristo anaongoza orodha. Mguso wa Mungu kwa mwanadamu umekuwa na utadumu kupitia kwa Yesu Kristo. Ijapokuwa Nafsi zote zatenda kazi kuokoa, ni Yesu pekee aliyekuwa Mwanadamu, akaishi na kufa kama mwanadamu kutuokoa. (Yoh. 6:47; Mt.1:21; Mdo. 4:12). Yesu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake (1Kor.5:19), hivyo naye aweza kuitwa mwokozi (cf. Tit. 3:4), kwa kuwa alituokoa kwa Kristo Mwokozi (Efe.5:23; Filp 3:20 cf. Tit. 3:6).

Mgawanyo wa kazi hufanya Nafsi tatu kutenda majukumu tofauti katika kumwokoa Mwanadamu. Jukumu la Roho Mtakatifu haliongezi chochote katika kutosha kwa kafara ya Kristo aliyoitoa msalabani. Kupitia Roho Mtakatifu, kafara ya msalabani inatumiwa na Yesu Mpatanishi anapoingia ndani ya muumini. Hivyo Paulo asema Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu (Kol. 1:27)

Lengo ni Wokovu (Focus on Salvation)

Kanisa la awali lilibatiza kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ni kupitia Yesu kwamba upendo wa Mungu na madhumuni yalifunuliwa, Biblia humlenga Yeye. Yesu ndiye kweli na njia na uzima (Yoh.14:6). Msalabani, Yesu alifanyika haki yetu, na utakaso na ukombozi (1Kor.1:30). Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu (Filp.4:7).